



COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA  
**THE HANSARD**

Tuesday, 11<sup>th</sup> February, 2025

**Third Assembly – Fourth Session**  
FIRST SITTING

*[The County Assembly met at 12:08p.m at the County Assembly Buildings]  
[The Speaker (Honourable Aharub Ebrahim Khatri) in the Chair]*

**PRAYERS**

**The Speaker** (Hon. Khatri): Honourable Members, you may be seated. Yes Clerk, next Order please?

**COMMUNICATION FROM THE CHAIR**  
OPENING REMARKS FOR THE FOURTH SESSION

Good morning Honourable Members. Honourable Members, I welcome you all back to this August House after a well-deserved recess which has allowed our personal renewal, we therefore reconvene today with a renewed sense of purpose ready to tackle the challenges and opportunities ahead in service to the people of Mombasa. Our constituents eagerly await our return to business, trusting us to shape the future, address complex issues and fulfil our commitments. Honourable Members, the challenges before us are significant, ranging from urban planning, health care and the cost of doing business to the deteriorating public transport sector and the provision of reliable water and sewerage services. These issues fall squarely within our constitutional mandate. We must utilize our legislative tools, both in Plenary and Committee to ensure the County Executive delivers quality, affordable and reliable services. This session must serve as a call to action, requiring us to work collaboratively with the County Executive to enact necessary legislation, policies and initiatives that will positively impact our Constituents. To achieve this, I urge you all to prioritize civility by engaging in an open and constructive debate, recognizing the validity of deferring viewpoints while striving for consensus. In addition, I urge us to, remain accountable to the people by ensuring every decision we make has a direct impact on our constituents. Let us ensure that every vote, debate, and Bill is guided by the principle of serving the greater good. Honourable Members, as we commence this session; I emphasize the urgency of concluding pending business to ensure an effective legislature, we are continuously assessed by our constituents and our performance will define their trust in us. Before the recess, the Assembly passed several key Bills and regulations:

1. The Mombasa County Ward Equitable Development Bill, 2024.

The Governor has referred it back with amendments under Standing Order 134, (3). The Assembly must now consider the amendments or reaffirm the Bill as initially passed.

2. The Mombasa County Multi-Year Project Financing Bill, 2024 - Sponsored by Honourable Kibwana Swaleh
3. The Mombasa County Village Administration Bill, 2024 - Sponsored by Honourable Jactone Madialo
4. The Mombasa County Ardhi Fund Regulation, Public Finance Management, 2024 - Sponsored by Honourable Maryam Baimu.

Honourable Members, several Bills remain pending. I direct the relevant Committees to conduct pre-publication scrutiny and ensure the timely processing of those approved for publication. I call upon all the Committee Chairpersons to rise to the occasion and expedite pending business. Honourable Members, legislation is at the core of our mandate and our performance is evaluated not only by the public, but also by oversight bodies such as the Auditor General, the Commission of Revenue Allocation and the Senate. While there are numerous legislative proposals, we must continue originating innovative ideas to address service delivery challenges in the County.

Honourable Members, I encourage Members to utilize the Secretariat provided by the Office of the Clerk to refine and submit legislative proposals. Likewise, I urge the Office of the Clerk to expedite the processing of these proposals. Honourable Members, to enhance our effectiveness, I urge all Members to actively participate in Plenary and Committee sittings as these are the primary forums through which we execute our legislative responsibilities. Additionally, the County Assembly has embarked on major infrastructural projects, including the construction and upgrading of the Assembly buildings to enhance our working environment and institutional capacity.

Honourable Members, my office will continue to facilitate your work and introduce initiatives that benefit the residents of Mombasa; one such initiative is the Mombasa Food Festival which celebrates our rich cultural heritage and local entrepreneurship. This festival has positioned Mombasa as a vibrant food tourism hub, creating economic opportunities for small businesses, chefs and vendors. By promoting our diverse cuisine, the event attracts local and international visitors, boosting tourism and strengthening our County's economy.

Beyond celebrating our culture, my office has also played a pivotal role in securing employment opportunity abroad for our youths in the program dubbed *Iko Kazi Abroad*. We have spearheaded programs that equip young people with the skills and networks needed to secure jobs internationally. Through these initiatives, many of our youths have been able to access meaningful employment, improving their livelihoods and contributing to our economy. Honourable Members, in addition to these County-wide initiatives I am humbled to share that yours truly was Honoured with the Judge's Choice Award at the Kenya Young Members of County Assembly Vanguard Awards as the Speaker of the Year, 2024.

*[Applause]*

Honourable Members, this recognition is not just a personal milestone, but a reflection of the collective efforts of this Assembly in upholding good governance, transparency, and commitment to the services. Let this award serve as a reminder that hard work, dedication, and service to the people never goes unnoticed. Honourable Members, as we are all aware; we are drawing closer to the end of our term, our electorates will evaluate our performance by the impact we made to their lives during this term. Therefore, as we embark on this new session, let us remain focused, united, and committed to the well-being of the people we serve, the people of Mombasa are looking to us for strong leadership, impactful policies and innovative solutions. It is our duty to ensure that every decision we make directly benefits and uplifts our communities. With these few remarks, Honourable Members I officially welcome you to the fourth session of the third Assembly, Karibuni sana.

*[Applause]*

Yes Clerk, next order, please?

### **PROCEDURAL MOTION**

#### ADJOURNMENT OF THE COUNTY ASSEMBLY

Yes, Honourable Athman Mwamwiri, Leader of Majority Party?

**The Leader of the Majority** (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, naomba kuleta Hoja kwa mujibu ya Hoja ya nidhamu sehemu 30 ya Kanuni zetu za kudumu, Bunge hili liweze kuhairisha vikao vyake leo hadi juma lijalo. Niombe Mheshimiwa Naibu wa Spika kuunga mkono Hoja hii.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Nasimama kuunga mkono.

**The Speaker** (Hon. Khatri): Thank you very much, Honourable Fadhili Makarani, Deputy Speaker and Honourable Athman Mwamwiri. Honourable Members, I now propose a question that the Motion by Honourable Athman Mwamwiri on the Adjournment of the County Assembly be considered by this Honourable House in the same terms as moved.

*[Question proposed and agreed to]*

Yes, Honourable Athman Mwamwiri, Leader of Majority Party, please make your contribution to the Motion.

**The Leader of Majority** (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika awali ya yote niregeshe shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu aliyeweza kutukutanisha tena siku ya leo na Waheshimiwa wenza tukiwa wote buheri wa afya, hii ni shukurani kwake. Mheshimiwa Spika, vile vile niombe Waheshimiwa kuweza kuunga mkono Hoja hii ya kuahirisha vikao hivi kwa sababu moja ya shughuli za urekebishaji wa Bunge letu zinaendelea na kwa sababu ya pita pita zetu kuna uwezekano wa kuhatarisha maisha yetu. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika kwa hali iliyofikia ni kwamba ndani ya siku chache mafundi wataweza kutamatisha zoezi hili na sisi kurudi katika mazingira tulivu na salama kuweza kusukuma gurudumu na kuhudumia wananchi wetu.

Lakini pia Mheshimiwa Spika kuna zoezi ambalo linaendelea, zoezi la kutafutia vijana kazi ama ajira za ughaibuni ambalo zoezi hili tunashukuru chini ya afisi yako na wale wasimamizi wamepeana fursa ya kwamba tuhamasishe vijana wetu zaidi waweze kujitokeza leo na kesho. Kwa hivyo hii pia Mheshimiwa Spika ni fursa kwetu ya kwenda kuhamasisha vijana wetu ambao hawakuweza kufika siku ya leo tuhakikishe kesho wamefika angalau kuangalia fursa hii na Mungu akitakabali iwe na wao wanaweza kupata riziki zao za halali katika nchi za ughaibuni. Kwa hayo Mheshimiwa Spika, ningepomba ya kwamba Bunge hili Waheshimiwa wenza tuweze tuafiki kuhairisha vikao hivi hadi tarehe 25/02/2025 ili tuhakikishe ya kwamba zoezi la marekebisho limekamili na ile fursa ya vijana wetu pia tumeweza kuitilia pondo. Kwa hayo mengi niunge Waheshimiwa kuweza kuunga Hoja hii. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Speaker** (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Fadhili Makarani, Deputy Speaker please make your contribution.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii. Mheshimiwa Spika, mimi pia nimesimama kuunga mkono; kwanza kabla niendeleo na kuunga mkono Hoja hii mimi nakupa pongezi kwa tunu uliotunukiwa kama Kiongozi wa Bunge letu la Mombasa, kuweza kupata tunu ile ni sote wana Mombasa tumepata tunu ile. Vile vile, Mheshimiwa Spika nazidi pia kutoa pole kwa Mheshimiwa mwenza ambaye aliweza kupoteza dadake wakati wa likizo, Mheshimiwa Mwenyekiti wa chama chetu cha Orange Democratic Party (ODM); na wale wengine ambao pia waliweza kupata majanga wakati wa huu msimu ambao tumekuwa tumepumzika mimi pia nawapa pole.

Mheshimiwa Spika nikirudi katika Hoja yetu, mimi naunga mkono Hoja iliyoletwa mbele yetu na Kiongozi wa Walio Wengi; nafikiri tukiangalia tunaona kuwa kweli kuna ujenzi ambao unaendelea katika Bunge letu na hali ya usalama ni vizuri kuwa tukiwa maana hata mimi nilipokuwa naingia nilipata kuna mabamba yale pale chini ilikuwa karibu nijikate. Kwa hivyo naona iko haja ya kazi ile iendeleo pasi na Waheshimiwa kuwa hapa na vile vile Mheshimiwa Spika tumepata hili jukumu la kuangalia vijana wetu hii ajira ambayo iko mbele ikiwa tutapata fursa ya kuwa pamoja sako na bako. Na vijana wetu wakitoka hapa katika lile zoezi linaloendelea kuna wale wengine ambao tutarudi kule chini mashinani ili tuzidi kuwapa mazoezi ya magari yale ili ikiwa wamefaulu wakienda kule wawe watapeleka sifa nzuri ya jina lako na jina letu. Hii ni kwa sababu umetupatia ratiba ya kuwa pia mbeleni watazidi kuja kutupatia sisi wana Mombasa ajira kama zile na ni vizuri sana kwetu.

Mheshimiwa Spika, nikimalizia twajua pia kuna mkutano mkuu upo nafikiri kama sijasahau wiki ijayo ambao uliitwa na County Assembly Forum (CAF) kuanzia tarehe 18/02/2025 kama sikusahau pia tukiongezea jambo kama lile kupitia afisi yako nitaungana na Kiongozi wa Walio Wengi ili tuweze kupangilia mambo yote tusije tukapatwa hatujajipanga. Kwa hivyo naunga mkono Hoja iliyoletwa mbele yetu na Kiongozi wa Walio Wengi na tarehe pia aliyotoa ya sisi kutoka Bunge hapa na kuweza kupanga kurudi Mheshimiwa Spika mimi naunga mkono na naomba Waheshimiwa waweze kuunga Hoja ambayo iko mbele. Ahsante.

**The Speaker** (Hon. Khatri): Thanks, Honourable Fadhili Makarani Deputy Speaker. Yes, Honourable Prischillah Mumba?

**The Chief Whip** (Hon. Mumba): Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza nasimama kusimama kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii na wakati huu mwema ambao tumetoka likizo. Ilikuwa ni likizo ndefu na tumeweza kurudi tukiwa wazima, pili nimesimama pia kupongeza juhudi zako Mheshimiwa Spika.

Vile vile kwa tuzo uliopata; tatu, kama vile mwenzangu alivyonukuu akasema anawapa pole kwa wale waliopoteza wapendwa wao nikiwa mmoja ni mimi ambaye nilimpoteza Mama mkubwa na wale walikuwa na wakati mwafaka tunashukuru Mungu. Mimi nimesimama kweli kuunga kweli jambo hili mkono kwa sababu ya kuwa tunajukumu kubwa la hizi siku mbili la kuweza kusaidia watu wetu waweze kupata ajira ambazo Mheshimiwa Spika umeweza kutusukumia na tuweze kuinua nyuso zetu katika Wadi zetu. Maana kusema kweli kwa hakika bila kuwa na wasiwasi na kuogopa hili ndio litakuwa ni jambo la kwanza la kutuinaa uso kwa ajili ya ajira. Maana ikiwa nitaweza kuchukuliwa hata watu watatu ama wanne huko kwengine hata huyo mmoja yuwateteleka; sasa ikiwa tumepata huku ambapo watu wetu tuko mia fil mia na hatuna tashwishi maana yake tumeona tayari kuna watu wameshaanza kuchukuliwa na tunaona mikakati iko wazi mbele ya macho yetu maana yake hata huo ukaguzi twaenda twauona unavyokwenda.

Mheshimiwa Spika twakupongeza kwa jambo hilo sana maana hakuna kitu kimefanywa cha *kibin maswali* cha chini chini ambacho hatukuelewa kinachoendelea; umefanya vizuri kuweka mahali wazi na macho yetu tunaona kila kitu hatuoni ukora wowote unaendelea pale, hatuoni kuwa kuna ukabila, hatuoni kuwa kuna udini, hatuoni kuwa kuna urangi, twaona kila kitu kinaenda sawa kwa sawa. Kwa hivyo sisi Waheshimiwa tunavyotaka ili tusiwe tuwe na tashwishi ya jambo lolote linalotendeka katika Kaunti yetu. Tunapongeza katika kazi hiyo na juhudi yako Mheshimiwa Spika na Mwenyezi Mungu azidi kukuongoza kwa sababu Jumba hili nafikiri hapo tulipofika sasa twategemea uzito wako kuweza kusogea kule kunako bakia. Kwa sababu hata ukajenga barabara, hata ukaweka mataa, hata ukafanya miradi mingapi ikiwa nawaambia Waheshimiwa hutaajiri rafiki yangu hapo tuko matatani. Ajira ndio kitu kinachotakiwa saa hizi, mtu atakwambia mimi sili barabara, mimi sili taa, mimi sili nini lakini lau tukipata watu wetu hata wanne ama watano umeingia katika Wadi yako ukisema hawa ndio nimepeleka katika nchi za ughaibuni kwa ajili ya kazi za mikono hakika nawaambia katika hizi siku mbili ikiwa huo ushindi utatoka nao Mama Ngina utakuwa umegeuza katika asilimia 75 katika kura za Wadi yako. Na ndio maana tunasema ni heri twende pale tukafanye ile juhudi ili watu wetu waweze kupata ajira, ajira kwa vijana ni kitu muhimu sana na huku kwetu saa hizi kazi zimekuwa ni nadra hakuna tukipata kama hivi tunashukuru. Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana na sote ni twendeni pale tukaweze kuhakikisha tumesukuma angalau watu wetu waweze kupata ajira. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Speaker** (Hon. Khatri): Thank you Honourable Prischillah Mumba Majority Chief Whip. Yes, Honourable Morgan please give your contribution?

**The Leader of Minority** (Hon. Matsaki): Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza kwa kunipa fursa hii, pili nashukuru Mwenyezi Mungu na karibuni Waheshimiwa wenza kwa kufunguliwa kwa hili Bunge leo na tatu namshukuru Mwenyezi Mungu tena kwa sababu ya hizi nafasi ambazo Mheshimiwa Spika ametupatia si rahisi unajua anayekuenzi muenzi na ni vyema zaidi vile ambavyo tumeamua kwanza kufunga Bunge letu kwa muda kwa ajili ya watu wetu na ajira kama vile Mheshimiwa mwenza alivyoweza kuzungumza. Kwa hivyo tuchukue nafasi hii twende tukajaribu kusukuma watu wetu waweze kupata nafasi hii ninajua ni vita lakini ni heri nusu shari kuliko shari kamili. Kwa hivyo tuchukue nafasi hii Waheshimiwa tuhakikishe tunafika pale watu wetu wanachukuliwa sifa itakuwa ni kwa Mheshimiwa Spika kwa sababu ya nafasi hizi na tuzidi kumuomba Mungu ampatie umri mrefu na iwezekane ya kwamba nafasi ziwe zaidi na zaidi kupata. Kwa hivyo mimi pia naunga mkono Hoja hii kuweza tuahirishe vikao kwa hivi sasa. Ahsante Mheshimiwa Spika.

---

**The Speaker** (Hon. Khatri): Yes, Honourable Mwamwiri you may reply to the Motion?

**The Leader of Majority** (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, nishukuru Waheshimiwa wenza kuweza kuchangia kwa hali ya chanya ya Hoja hii lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuweza kutukumbusha kuhusiana na kongamano la Mkutano Mkuu utakaofanyika katika Jiji la Nairobi Ukumbi wa KICC kuanzia Juma lijalo ambalo litaanza kuanzia tarehe 19 rasmi. Kwa hivyo kusafiri ni tarehe 18 niwakumbushe tu Waheshimiwa ni kongamano hili ni la Waheshimiwa Wawakilishi wa Wadi wote Kenya nzima ambalo watajadili masuala nyeti yanayotusibu sisi kama Wawakilishi chini ya usimamizi wa CAF, ikiwemo mishahara ya MCAs ambayo tunalipwa hapa Kenya ikiwa ni dhulma. Vile vile pia kujadili suala ambalo Mabunge yetu yanapitia baada ya Tume ya kusimamia migao ya rasilimali ya Kaunti kuweza kutukata pesa nyingi sisi kama Mabunge kutufanya kukosa nguvu kusimamia suala la usaraangi ama *oversight* katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Pia vile vile kunalo suala la kuwekeza ama kutengenezwa kwa ile sheria ya usimamizi wa maendeleo katika Wadi zetu ama *Ward Fund* na mustakabali wetu baada ya kuhudumu kama Mwakilishi wenzetu Wabunge wana marupurupu ya *retire*; wakienda *retire* wako na *pension* pesa ya uzeeni lakini sisi Wawakilishi tumeshuhudia ndugu zetu waliotutangulia baada ya kutoka kwa nafasi hizi wakisambaratika na kuwa maskini wa kutupa kwa sababu rasilimali zao, nafasi zao walizitumikia katika kuhudumia wananchi. Kwa hivyo haya ni yale yatakayojadiliwa kule nisisitize Waheshimiwa sisi chini ya ofisi ya Mheshimiwa Spika akitupatia ruhsa na kutuwezesha kwenda tufikeni kwa wingi ili tuweze kufanikisha ajenda. Nawashukuru sana Waheshimiwa lakini pia turudi na hili suala la kazi ughaibuni tuhamasishe vijana wetu kisawa sawa sababu tamati ni kesho kuingia tuone na sisi tumechangia kubadilisha maisha ya watu wetu. Ahsante na Mwenyezi Mungu atubariki.

**The Speaker** (Hon. Khatri): Thank you Honourable Athman Mwamwiri, Leader of Majority Party. Honourable Members, I stand to put a question the Motion by Honourable Mwamwiri on the Adjournment of the County Assembly be adopted in this Honourable House in the same terms as moved.

[Question put and agreed to]  
[Applause]

Yes, Clerk next Order please?

### ADJOURNMENT

Honourable Members, this House stands adjourned until 25<sup>th</sup> February, 2025 at 10:00a.m.

The House rose at 12:46p.m.